# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO -MASWALA YA JAMII

## KIPINDI CHA NNE "NDOTO YANGU SI YA KUUZWA"

**MWANDISHI: CHRISPIN MWAKIDEU**

**MHARIRI: ANDREA SCHMIDT**

**WAHUSIKA: Eveline (19),Mapito (40), Roni (14), Mjumbe (55), Beti (12), Wanafunzi mseto (12+)**

**Msimulizi:**
Hujambo msikilizaji popote pale ulipo na karibu tena katika kipindi kingine cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu maswala ya jamii - Jinsi gani unavyoweza kuingia na kuchangia katika siasa. Katika kipindi kilichopita tulimuona Beti akitahiniwa kwa mara ya kwanza kama kiongozi wa kikundi chake cha uimbaji. Eveline na wenzake walifanya kazi ya kusaidia jamii na kuungwa mkono na wakaazi, lakini mbunge alimbeza akisema bado ni msichana mdogo na hawezi kufaulu. Karibu katika kipindi cha leo "Ndoto yangu si ya kuuzwa"

**Onyesho la Kwanza: Makazi ya Mapito**

**SFX: SIMU YA RUNUNU YALIA**

**1.BETI**: Eve! Eve! Simu yako ya mkono inalia..

**2.EVELINE:** Haya hebu ilete...hello! hello! (**kwa sauti ya juu**), HELLO! Ala!hajibu, labda mtu ameghaflika akapiga nambari yangu kimakosa. Iregeshe iendelee kuchaji.

**3.BETI:** Eve, kwa nini watu wengi wanawachukulia wanasiasa kuwa wezi na waongo?

**3.EVELINE**: Sio sawa kujumulisha wanasiasa wote kuwa wezi. Nadhani

inategemea na malezi ya mtu. Aliyekulia tabia hiyo bila shaka ataiendeleza iwapo atapata mamlaka mbeleni.

4.BETI: Mimi pia nilifikiria hivyo na ndivyo hususan nilivyowaeleza wenzangu katika kikundi cha uimbaji. Eeh wacha niwahi shule nisipo kwenda kutazuka la kuzuka, kwa maana kuna msichana mmoja huyo mkaidi sana katika hiki kikundi, sijui yuatakaje..haya kwaheri.

**SFX: MLANGO UNABISHWA .. CHUMBANI MWA MAPITO**

5.RONI: Ni mimi Baba..niingie?

6.MAPITO: Ingia! Ah Roni, sote tunakerwa sana na kubadilika kwako hivi punde. Si kawaida yako kutokua mchangamfu. Kunani?

7.RONI: Baba najihisi kama niliyekosa umuhimu wa kuishi. Nilijitolea kwa dhati katika timu yangu lakini mkufunzi hakunichagua mimi kama nahodha wa timu badala yake alimteua Samu.

8.MAPITO: Sasa Mwanangu, shida iko wapi? Heh? Shida ni kuwa wewe hukuchaguliwa au ni kuwa Samu alichaguliwa badala yako?

9.RONI: Yote mawili baba. Nilijitolea zaidi katika timu. Sikukosa mazoezi, nikatii amri zote, kwa nini wanifanyie hivi? (**kwa huzuni tele**)

10.MAPITO: Roni, sijawahi kumweleza yeyote haya isipokuwa marehemu mama yako. Wajua mimi sikupanga kuwa askari polisi.nilipokua kijana nilipenda sana michezo ya riadha na zile shahada ulizo ziona ni thibitisho. Niliposhindwa katika michujo ya kitaifa.. nilihisi kana kwamba nilisalitiwa na ndiyo ikawa hatima yangu mimi na riadha hizo.Sasa ninafukuzana na wezi na wanyan'ganyi. Ndiyo sababu sikutaka ucheze mpira wa miguu, nilidhani kuwa huenda makosa yangu yakawa yako. Lakini nilikuwa nimekosea. wewe una maisha yako na pia haki ya kujiamulia, kwa hiyo rudi kiwanjani, ukawajibike.

11.RONI: Sikujua hayo..lakini Baba siwezi kurudi..wachezaji wenzangu watanicheka.

12.MAPITO: Mambo ya watu yasikufanye ukakosa kutimiza lengo lako. Waache wacheke lakini hatimaye watakupata kileleni.

13.RONI: Sawa..nitalifikiria sana wazo lako. nashukuru sana Baba. Acha nikimbie shule.

**SFX: SIMU YA EVELINE INALIA TENA**

14.EVELINE: Ndio..Hello..HELLO!

15.MJUMBE: Huyo ni Eveline Mapito?

16.EVELINE: Naam! Nani mwenzangu?

17.MJUMBE: Vyema. Mimi ni Mheshimiwa Mbunge wa Milimani. nilipata nambari zako za simu yako ya rununu kutoka kwa rafiki zako. Ningependa kukualika kwa chakula cha mchana au kikombe cha kahawa..jinsi upendavyo leo jioni. Unasemaje?

18.EVELINE: (**Akitatizika**) Aaah..sijui..labda niombe kukuuliza.. lengo la mwaliko huu Mheshimiwa… ni lipi?

19.MJUMBE: Siwezi kukueleza katika simu..Kwa nini tusikutane mkahawa wa Diners kama saa saba hivi? Nitakueleza kila kitu.

20.EVELINE: Mheshimiwa, bado niko na hofu..na sijui kama..

21.MJUMBE: Usihofu kamwe, nitakusubiri.

22.MSIMULIZI**:** Naam, mtego ulikuwa ushategwa,chambo kimewekwa katika ndoano. naye Eveline alihitajika kufanya maamuzi ya dharura.

**<u>Onyesho la Pili: Katika mkahawa wa Diners</u>**
**SFX: MUZIKI MORORO AINA YA `JAZZ` UNASIKIKA**

1.MJUMBE: Ah Eveline..shukran kwa kufika.tafadhali kaa na uagize chochote unachotaka.

2.EVELINE: Nashukuru Mheshimiwa, lakini sitakunywa chochote.

3.MJUMBE: Kumradhi..usiniite Muheshimiwa,hapa hatuko kazini au ofisini tuko katika maeneo ya kujivinjari.

4.EVELINE: Muheshimiwa..labda ungenieleza maudhui ya kunialika hapa.

5.MJUMBE: Aste..aste..mmmh si makosa kunywa kikombe cha chai pamoja na mbunge wako. Hata hivyo kwa vile una haraka ya kujua, nimegundua umekuwa maarufu haraka sana katika siasa.. **(Amnong´onezea)** zniko tayarikukupa shilingi nusu milioni iwapo utajitoa katika kuwania udiwani hapa Milimani. Nusu milioni!!!!

6.EVELINE: (**Mshtuko**) Nusu milioni!?

7.MJUMBE: Nini tena, je hizo ni pesa kidogo? Sawa..nitakupa kipande cha ardhi katikati ya jiji..Wasemaje?

8.EVELINE: (**Mshangao**) Nusu milioni pamoja na ardhi ya bure hapa jijini!

9.MJUMBE: Hasa! Lakini hii iwe siri kati yetu.Isitoshe naweza kukuajiri kama msaidizi wangu katika maswala ya siasa. Si unajua kupiga chapa?

10.EVELINE: Samahani Muheshimiwa,lakini ari yangu siwezi kuiuza. Kufanya hivyo ni sawa na kuwasaliti watu wa eneo langu,nia yangu ni kuwa diwani wao.

11.MJUMBE: (**Akimtishia)** Eve unafanya makosa makubwa sana kwa kukataa hiyo ruzuku,pia unahatarisha maisha yako na ya jamii yako

12.EVELINE: Hunielewi mheshimiwa. Kwa kukubali hongo nitakuwa nakiuka maadili na imani yangu. Naamini mtu anaweza kufaulu kisiasa bila kuwa mfisadi.

13.MJUMBE: (**Kwa hasira tele**) Eti unaniita mimi mfisadi!?? Wewe mtoto Umwekwisha. Nitaukomesha huu upuzi wako unaouita siasa!

14.EVELINE: Sidhani mhemshimiwa. Nimenasa kila neno kupitia teknolojia ya simu yangu na lolote litakalotokea nitakuwa nimewajulisha askari kitambo!

15.MJUMBE: (**Sauti ya Hofu**) La! Usifanye hivyo..huko ni kuniumbua..eeh tafadhali nakusihi..nitafanya lolote kukusaidia.

16.EVELINE: Huwezi kunidanganya kwa sasa...

17.MSIMULIZI: Mbunge alijaribu kununua kile kisichokua na thamani ya pesa..alasiri hiyo hiyo..Beti alikuwa akifanya mazoezi ya kuimba katika kwaya..

**<u>Onyesho la tatu: Katika mazoezi ya uimbaji</u>**

**(WANAFUNZI WANAJIFUNZA WIMBO WA"MALAIKA")**

1.BINTI: Beti tumechoka sana..tungelipumzika kidogo.

2.BETI: Si tumeanza tu hivi punde,nitawaeleza wakati wa kupumzika ukifika

3.BINTI: Siwezi kujilazimisha kuimba nyimbo ambayo haileweki,kama nyinyi mwaimba basi imbeni weee mpaka koo ziwakauke. mimi napumzika saa hii.

4.BETI: Kwa nini wasema hivyo na tumeanza kuona maendeleo.Tafadhali usituvunje moyo,ukitaka kwenda wewe nenda lakini usirudi tena!

5.BINTI: Nyoo siendi popote!kwani hii kwaya ni yako?tena sikiza Beti wewe si mzazi wangu kunisomea au kuniambia ninalopaswa kufanya upo! hapo?

6.BETI: Sawa.. wangapi wanataka aende? Nyosheni mikono…

**KIMYA WOTE**

7.BINTI: (**Akimcheka Beti**) Hahaha...Beti pole..hukujua ya kwamba hawa ni rafiki zangu? Wananipenda mimi zaidi kuliko wewe…hahaha

8.BETI: Si neno..na kama imefikia hapo basi mutaamua nyinyi, ni yeye au ni mimi.Chagueni ela mkumbuke mashindano hayako mbali.

9.BINTI: Beti unataka mashindano na mimi ya kujua ni nani aliye bora? Wachekesha..kwani hujui hawa waimbaji wote wako kwa ajili yangu nikitoka na wao wanatoka.

10.BETI: Tutajua mbivu na mbichi leo..haya moja..naona mkono wa pili.. musiogope..endeleeni kuja kwangu.

11.BINTI: Mwengine yeyote atakaye vuka upande wake ajue yeye si rafiki yangu tena pia sitamualika kwenye beach party.

12.BETI: Hapana usirudi tafadhali..msikubali kudanganywa na pesa zake anawapotosha tu, hana nia nzuri na kikundi chetu.

13.BINTI: Kwa vile sote tumepata sita kwa sita..na tuko sambamba..hii ina maana siendi mahali niko hapa hapa (**anamkejeli Beti)**

14.MSIMULIZI: Haya mpendwa msikilizaji, Beti Mapito analazimika kuanza upya kukiunganisha kikundi chake cha uimbaji..Wakati huo huo, kule

katika kituo cha polisi, Mapito presha imempanda kwa hasira..

**<u>Onyesho la nne: Kituo cha Polisi</u>**

1.MAPITO: Kwa nini Eve!??ni kwa nini hukunieleza mwanzoni.hujui vile umenivunja moyo. Jinsi nilivyokuamini.

2.EVELINE: Baba..nilijua kama ningekuarifu ya kwamba naenda kukutana na Mbunge wetu labda ungelinikataza, ndiposa nikajiamulia.

3.MAPITO: (**Kwa hasira**) Peke yako sio? Ukaamua kujiamulia.na mimi? Si nilidhani ya kwamba mimi ni mshauri wako? Mbona ulinificha haya?

4.EVELINE: Baba..mimi ni mtu mzima sasa nina miaka kumi na tisa kisha isitoshe ninagombea kiti cha udiwani hapa kwetu. Itanilazimu nianze kufanya uamuzi peke yangu saa zingine na kuwajibika kutokana na maamuzi hayo.

5.MAPITO: Sasa hata ya kupata kiti..tayari umeanza kutupuuza, sio?ghafla tumekuwa hatuna maana tena kwako.umenikasirisha sana na sijui kama nitaweza kukusamehe! Hujashinda na mambo ni haya!

6.EVELINE: Baba tafadhali..(**Akiomba msamaha**)

7.MAPITO: Sina la ziada,tuonane nyumbani.hapa nina kazi chungu nzima za kufanya.

**SFX: MLANGO UNAFUNGULIWA NA KUFUNGWA KWA NGUVU**

**<u>MWISHO WA KIPINDI CHA NNE</u>**

**<u>Msimulizi:</u>**

Kwa kishindo hicho cha mlango ndipo tunakamilisha kipindi chetu cha nne

kuhusu maswala ya jamii - jinsi gani unavyoweza kuwa mshirika katika siasa. Usikose kujumuika nasi tena juma lijalo uone vipi vyombo vya habari vitakavyoripoti kutiwa mbaroni kwa mbunge na vipi timu ya kandanda itakavyohisi Roni atakaporudi tena uwanjani. Unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe Hadi wiki ijayo kwaheri.